**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SITA

## KIKAO CHA KWANZA

**31 JANUARI, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SITA

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 31 JANUARI, 2017

## I. WIMBO WA TAIFA:

## II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA TATU ASUBUHI:

## III. KIAPO CHA UAMINIFU:

Orodha ya Wabunge wanaoapishwa.

1. Mhe. Abdallah Majula Bulembo;
2. Mhe. Anne Kilango Malecela;
3. Mhe. Juma Ali Juma;
4. Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi.

## IV. TAARIFA YA SPIKA:

## V. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**1. MHESHIMIWA OMAR ABDALLAH KIGODA (HANDENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Handeni inahudumia Wagonjwa kutoka Kilindi, Mziha, Wegero na Handeni yenyewe:-

Je, ni lini Serikali itaipatia vifaa tiba na Wauguzi wa kutosha Hospitali hiyo.

**2. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya elimu vijijini kama nyumba za Walimu pamoja na kulipa malimbikizo ya madeni ya Walimu wanayodai Serikali.

**3. MHESHIMIWA ESTER ALEXANDER MAHAWE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Simanjiro haina Hospitali ya Wilaya na hivyo kusababisha mateso kwa wakazi wa maeneo mbalimbali ya Wilaya hiyo hususan Wanawake ambao wanakosa huduma za kujifungua lakini pia kutokana na uchache wa Vituo vya Afya na Zahanati:-

(a) Je, ni lini Serikali itavipa hadhi Vituo vya Afya vya Mererani na Orkesment ili kupunguza tatizo;

(b) Wilaya ya Simanjiro ina gari moja tu la Wagonjwa; Je, ni lini Serikali itapeleka gari jingine kwenye Kituo cha Afya Mererani ili kuokoa maisha ya akina mama wajawazito.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**4. MHESHIMIWA MUHAMMED AMOUR MUHAMMED (BUMBWINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Suala la usalama wa Raia na mali zao ni moja ya dhamana ya Jeshi la Polisi nchini; Ni muda sasa Zanzibar Wananchi wamekuwa wakipigwa, kunyanyaswa na kunyang'anywa mali zao na Vikosi vya SMZ:-

Je, nini Kauli ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusiana na matukio hayo huko Zanzibar.

**5. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Pamoja na kuwa Jimbo la Kigamboni ni Wilaya ya Kipolisi, majengo ya Ofisi ya Kamanda wa Polisi Wilaya (OCD) na Kituo chake ni chakavu sana:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha Wilaya hii inakuwa na Ofisi nzuri za Polisi;

(b) Je, hatua hizi zitaanza kutekelezwa lini.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**6. MHESHIMIWA RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Tatizo la kesi za ubakaji na ulawiti kwa watoto wadogo limekuwa likiongezeka siku hadi siku katika Mkoa wa Iringa:-

(a) Je, nini mkakati wa Serikali kunusuru hawa watoto wasiendelee kufanyiwa matendo haya ya kikatili;

(b) Je, ni utaratibu gani unatumika kushughulikia Watuhumiwa wa kesi hizi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**7. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Vijiji vya Kabage, Kungwi, Sibwesa, Kasekese na Kaseganyama viko kwenye mgogoro mkubwa wa ardhi na W. M.A:-

Je, ni lini Serikali itaingilia kati na kutatua mgogoro huo unaoleta usumbufu wa mara kwa mara.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**8. MHESHIMIWA SALOME WYCLIFFE MAKAMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Serikali kupitia Mawakala wake wa maji katika Mkoa wa Shinyanga imepandisha bei ya maji kwa takribani asilimia 100 kwa *unit* na *service charge*:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza bei ya huduma ya maji ili Wananchi waweze kumudu gharama za huduma hiyo, na pia kuwavutia zaidi Wawekezaji viwandani ili waendelee na uzalishaji.

**9. MHESHIMIWA DKT. MARY MICHAEL NAGU (HANANG'):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wilaya ya Hanang' ni moja ya Wilaya ambazo ziko katika Bonde la Ufa na hivyo upatikanaji wa maji ni wa shida sana; Suluhisho la kudumu ni kuchimba visima virefu na kujenga Mabwawa:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga bwawa la maji katika Kijiji cha Gidahababiegh ambalo lilibomoka kutokana na mvua;

(b) Je, ni lini Serikali itarudia kuchimba visima katika Vijiji vya Hirbadamu, Dajameda, Mwanga, Gidika, Lalaji na Wandela ambavyo awali vilipata ufadhili kupitia Mradi wa Benki ya Dunia lakini Maji hayakupatikana.

**10. MHESHIMIWA RISALA SAID KABONGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Mto Ruaha Mkuu unatiririsha maji yake katika Bwawa la Mtera na Kidatu kwa mwaka mzima kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**11. MHESHIMIWA BALOZI DKT. DIODORUS BUBERWA KAMALA (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Tulipoanza kutekeleza Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki, kuna bidhaa kutoka Kenya ziliwekwa kwenye Kundi ‘B’ ambazo zilikuwa zinatozwa kodi iliyokuwa ikipungua taratibu hadi ilifikia kiwango cha asilimia sifuri mwaka 2010:-

(a) Je, bidhaa hizo ziliongezeka kwa kiasi gani kuingia Tanzania kuanzia mwaka 2005 – 2015;

(b) Je, Viwanda vya Tanzania vinavyozalisha bidhaa za Kundi ‘B’ vilikabiliwa na changamoto

zipi kutokana na kuondolewa kwa kodi iliyokuwa ikipungua taratibu hadi kufikia asilimia sifuri mwaka 2010.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

**12. MHESHIMIWA DANIEL EDWARD MTUKA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Watanzania wengi wanahitaji umeme Mijini na Vijijini, lakini wanashindwa kuvuta umeme kutokana na gharama kubwa ambapo *Service line* ni sh 177,000/= na zaidi na gharama ya nguzo ni Sh. 337,740/= na zaidi:-

(a) Kwa kuwa nguzo ni mali ya TANESCO; Je, kwa nini nguzo hizo zisilipiwe na Serikali;

(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kupunguza "Service line costs" kuwa sh. 27,000/= kama ilivyo kwa mradi wa REA.

## WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

**13. MHESHIMIWA MUSA RASHID NTIMIZI (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Serikali iliahidi kujenga Viwanda mahali zinakopatikana malighafi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha tumbaku Mkoani Tabora;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha kusindika asali Mkoani Tabora.

**14. MHESHIMIWA CONCHESTER LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Serikali inatakiwa kuweka mkakati wa kuhakikisha mazao yanauzwa katika Vituo maalum vinavyotambuliwa ili kuzuia Walanguzi kufuata mazao shambani na kununua kwa bei ndogo:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kutunga Sheria kuzuia Walanguzi kwenda kununua mazao shambani.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**15. MHESHIMIWA OSCAR RWEGASIRA MUKASA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Matumizi yasiyo sahihi ya lugha ya Kiswahili kwenye Vyombo vya Habari hayatoi fursa ya kukua kwa lugha yetu na badala yake yanachangia kurithisha lugha yetu kwa Watoto kwa namna iliyo mbovu; Mathalani, Mtangazaji wa Runinga au Redio anasema "hichi" badala ya hiki au nyimbo hii badala ya "wimbo huu" n.k.:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kimkakati wa kuvifanya Vyombo vya Habari kuwa Mawakala wa kulinda usahihi wa lugha ya Kiswahili badala ya kuwa miongoni mwa wabomoaji wa lugha yetu.

**VI. KAULI ZA MAWAZIRI:**

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

## VII. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wa Mwaka 2016 *[The Legal Aid Bill, 2016].*

**DODOMA**
**31 JANUARI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**